



Cour  
Pénale  
Internationale

International  
Criminal  
Court

ICC-PIDS-FS-03-002/09\_Swa

# Biro ya Prokirere



Mwendesha mashtaka, Luis Moreno-Ocampo na wendesha mashtaka makamu, Fatou Bensouda

Picha: ICC-CPI/Wim van Cappellen

**B**iro ya Prokirere ni moya ya pande ine ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Inaongozwa na Prokirere, Luis Moreno-Ocampo, aliyechaguliwa na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama, na ana uwezo wote ya menejimenti na uongozi ya Ofisi hii, ikiwemo uongozi ya wafanyakazi, ya vifaa na bitu bingine. Prokirere, alianza kazi tarehe 16 mwezi wa sita mwaka 2003.

Biro ina kazi ya kupokea na kuchambua ripoti na habari ili kuazimu kama kuna msingi ya maana kwa kuanza uchunguzi, kuendesha uchunguzi katika mauaji ya halaiki, makosa ya jinai juu ya binadamu na makosa ya jinai ya mu vita na kuwapeleka mbele ya Mahakama benye balitenda makosa hayo ya jinai.

Ikiendesha uchunguzi na mashtaka, Biro ya Prokirere inaleta mchango wake juu ya kutimiza shabaa ya Mahakama, ambayo ni kusaidia kukomesha hali yakutolipiza batendaji ya makosa ya jinai ya buzito sana yenyi kuangalia ulimwengu wa kimataifa yote muzima, na kusaidia hivi kuepuka makosa hayo ya jinai.

Kutokana na kazi yake, Biro la Prokirere inaundiwa na *division* tatu :

- *Division* ya uchunguzi inakazi ya kuongoza uchunguzi (kwa mfano kukusanya na kuchambua ushuhuda, kuuliza batu benye kuhusika na uchunguzi na pia wateswa na mashahidi). Kwa hiyo, na kwa ajili ya kuonesha ukweli, Mkataba inalazimisha Biro ya Prokirere kufanya uchunguzi kuhusu mambo yanayo semeya mushtakiwa na yale yanayo mushtaki.
- *Division* ya mashtaka, inakazi ya uchunguzi, na

itakuwa pia na kazi muhimu mu mwenendo za kesi mbele ya Vyumba mbalimbali vya Mahakama.

- *Division* ya mamlaka, kukamilishana na ya uhusiano inafanya uchambuzi ya ripoti na habari, ikipewa msaada kutoka *division* ya mashtaka, inajifunza hali ya kukubaliwa kwa mashtaka na inasaidia kuweka ushirikiano unaofaa katika kazi za Biro.

**P**rokirere anaweza kuanzisha uchunguzi kutokana na hali ambayo imeletwa na moja wa Nchi zinazounda Mahakama wala na Baraza ya Usalama likilingana na hatari ambayo inaweza kuleta amani na usalama ya kimataifa. Tena, Prokirere anaweza, kwa niaba yake mwenyewe, kuanza uchunguzi katika eneo ao kuhusu raia wa moja wa Nchi zinazounda Mahakama ambao utahakikishwa na Chumba ya utangulizi ya Mahakama.

Ni siasa ya Biro ya Prokirere kuelekeza uchunguzi wake kwa batu bote benye kuwa na jukumu kubwa ya makosa ya jinai yaliyotendeka katika hali ambayo inachunguzwa. Utangulizi ya Mkataba wa Roma inatambua kwamba Mahakama yenyewe ni fasi ya mwisho kwa kuwapatia haki wateswa wa mauaji ya halaiki, wa makosa ya jinai ya mu vita na wa makosa ya jinai juu ya binadamu. Kwa hiyo Mkataba wa Roma unapatia Mahakama na Biro ya Prokirere kazi ambayo inakamilishana na kanuni ya sheria ya taifa.

Mkataba wa Roma inasema tena kwamba Biro ya Prokirere ni huru katika kazi zake. Kutokana na hiyo, mfanyakazi wake hawezi kuomba ao kutumika kulingana na maagizo kutoka nje kama vile kwa nchi, kwa mashirika ya kimataifa, kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ao kwa watu wazima.



**Luis Moreno-Ocampo, Mwendesha mashtaka:** Tarehe 21 mwezi wa ine mwaka 2003, Baraza la Nchi zinazounda Mahakama ilimuchagua bwana Luis Moreno-Ocampo kutoka Ajentina kama Prokirere wa kwanza wa Mahakama hii. Ana ujuzi enye sifa katika kazi ya Prokirere, ya mwakilishi, ya mwalimu wa chuo kikuu na wakupanga mambo ya kisheria kuhusu maswala ya sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai, ya sheria ya haki za binadamu, za kupiganisha rushwa na za utetezi wa maandishi wa habari. Mwaka 1984, aliongoza uchunguzi katika kesi ya makamanda wakuu kenda wa jeshi, ikiwemo marais watatu wa zamani, bote balikuwa viongozi wa kijeshi balioongoza Ajentina tangu mwaka 1976 mpaka mwaka 1980. Masambo iliyofuata, ambamo tano kati ya washtakiwa walihukumiwa, ndio ilikuwa ya kwanza ya batu banaoshtakiwa kwa mauaji ya batu bengi tangu kesi ya Nuremberg ya bakubwa ya chama cha Nazi. Katika uendeshaji ya kesi hii, bwana Moreno-Ocampo alitoa neno juu ya mashtaka 700 ya "mauaji, utekaji nyara na mateso", aliita mashahidi 835 na alisoma maelfu ya makartasi. Baada ya hayo, alifungua mashtaka ya wale waliohusika katika mauaji ya watu wengi wakati wa mauaji ya kijeshi wa miaka 1987 na 1992 nchini Ajentina. Miaka kumi kisha kesi ya wanajeshi 'Junta Trials', bwana Moreno-Ocampo alianza kutumika mu ma kesi za hali ya juu katika sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai, ikiwemo kurejesha kwa nguvu kwa mukubwa wa zamani wa chama cha Nazi Erich Priebke nchini Italia; kesi ya polisi ya siri ya Chile kuhusu mauaji ya general Carlos Prats na kesi ya makamanda walioshtakiwa kutenda matendo mabaya kazini wakati wa vita vya Malvinas/Falklands. Bwana Moreno-Ocampo alikuwa mwanamemba wa *global board of Transparency International*, na profesa katika vyuo vikuu vya Stanford na Harvard.



**Fatou Bensouda, mwendesha mashtaka makamu (mashtaka):** Tarehe 8 mwezi wa kenda mwaka 2004, bibi Bensouda kutoka Gambia alichaguliwa kama Prokirere makamu na Baraza la Nchi zinazounda Mahakama. Yeye ni mkuu wa *Division* ya mashtaka katika Biro ya Prokirere. Mbele ya kuchaguliwa kwake, bibi Bensouda alifanya kazi kama mshauri wa kisheria na kama mwakilishi kwenyi Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Rwanda (ICTR) mjini Arusha nchini Tanzania, akapandishwa cheo mpaka kuwa mshauri mkuu wa kisheria na mkuu wa *Unite* ya ushauri wa kisheria. Mbele ya kufanya kazi katika Mahakama ya Kimataifa ya jinai ya Rwanda, alikuwa manaja mkuu wa benki moja ya biashara nchini Gambia. Kati ya miaka 1987 na 2000, alikuwa Prokirere mkuu wa serikali (*Senior State Counsel*), Prokirere wa serikali (*Principal State Counsel*), mkubwa makamu wa mashtaka, msaidizi wa Prokirere (*Solicitor General*), secretaire general wa Jamuhuri (*Legal Secretary of the Republic*), Prokirere mkuu (*Attorney General*) na waziri wa sheria, wakati enye alitumika pia kama mshauri mkuu wa kisheria wa Rais na wa Baraza la Mawaziri wa Jamuhuri ya Gambia. Bibi Bensouda alishiriki pia kwenyi mazungumuzo kuhusu Mkataba wa umoja wa kiuchumi ya Nchi za Afrika ya magharibi (ECOWAS), Bunge ya Afrika ya magharibi, na Mahakama ya umoja wa kiuchumi ya Nchi za Afrika ya magharibi. Alikuwa pia mjumbe katika mikutano ya Umoja wa Mataifa ili kuzuia mauaji, katika mikutano ya mawaziri wa Shirika la Umoja wa Afrika kuhusu haki za binadamu, na mjumbe wa Gambia kwenye mikutano ya Komisheni ya matayarisho ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Bibi Bensouda ana digrii ya masomo ya juu (*masters degree*) katika sheria ya kimataifa ya bahari na sheria ya uziwa, na kwa hiyo yeye ndiye mwanafunzi wa kwanza wa sheria ya kimataifa ya bahari nchini Gambia.

